# MWISHO USIOJULIKANA

Gerhard Nehls

03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 1 30-10-2021 20:52:02

Original Title: Destination Unknown

This is a publication of
Life Challenge © SIM 2021
P.O. Box 50770-00200,
Nairobi, KENYA
**info@lifechallenge.de**

All rights reserved. No part of this book may be reproduced without written permission, except for brief quotations in books and critical reviews.

Translation: John Augustine Mabutagulwa, Zanzibar, Tanzania

Printed and bound in Kenya

# Mwisho Usiojulikana

Lengo la kila dini ni maisha ya milele ya mwanadamu. Itakuaje tukifa? Tutakwenda wapi? Huko kutafananaje? Tunawezaje kujua hatima yetu? Kuna ufahamu wowote wa hakika kuhusu swala hili? Maswali haya na mengine mengi muhimu na makali hutolewa kwa waalimu wa dini - na hujibiwa kwa njia tofauti tofauti!

Cha kusikitisha ni kuwa dini iliyorasimishwa huanza kufundisha dini kwa watu ambao huwa hawajauliza maswali haya. Baadaye kidogo, “akili ikidhibitiwa”, mara nyingi taarifa iliyotolewa huwa haihojiwi tena. Hisia ya wengi na utii wao huzuia wazo huru, na badala ya mtu kutafuta na kuchunguza kwa makini, hoja hubuniwa kuimarisha msimamo wa mtu binafsi na huipuuza mitazamo mingine. Misingi yote ya ushawishi wa mtu binafsi huthibitiwa, na makosa yote hulundikwa kwa wenye mitazamo tofauti. Badala ya kuuangalia ushahidi wote na kufikia uamuzi kwa akili iliyo wazi yenye utulivu na busara, mara nyingi hutangulizwa ushawishi!

Ushawishi kama huo ni hatari linapokuja suala la kuamua hatima ya mtu ya milele, maana hakuna marekebisho yanayoweza kufanywa baada ya mtu kuyaacha maisha haya. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa makini sana. Katika ari hiyo, hebu tuchunguze mada ya kuvutia kabisa.



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 1 30-10-2021 20:52:02

## JE TUNA UHURU WA KUCHAGUA AMA TUFUATE TU YALIYOAMRIWA?

Yote tunayoweza kujua kuhusu Mungu ameyafunua katika Neno Lake. Tunaweza kuyaona matendo Yake. Mtu hawezi kuuona upepo, ataona tu yanayotendeka, hivyo tunaweza kuutambua uwepo wake kwa imani. Tunaweza pia kuchagua tu dhana kuwa yote yaliyopo na yanayotokea ni kwa bahati!

Wale wanaomwamini Mungu wanakabiliwa na chaguo lingine. Huenda likaonekana kama ni upuzi, lakini hebu tulifikirie kwa muda. Lazima "tuamue" kama ni Mungu pekee anayeweza kutenda, au kama alimpa mwanadamu uhuru wa utashi na utendaji.

Kama tuna utashi huru wa kuchagua tunachotaka kufanya, ni wazi kuwa tunawajibika kwa matendo yetu. Kama hatuna chaguo katika suala hilo, kama Mungu ndiye chanzo cha matendo yetu yote - basi yeye ndiye wa kuwajibika. Kwa hali hiyo, kama yeye ni mwenye haki, na lazima tusadiki hivyo, hataweza kutuadhibu kwa kosa lo lote la kutenda, kusema, au kufikiria.

Mwanatheolojia wa Kiislamu wa zamani anayejulikana sana Risaleh-i-Barkhavi anasema hivi kuhusu Mungu:

> "Siyo tu kwamba anaweza kufanya kila jambo, yeye ndiye pekee anayefanya kila jambo. Mtu anapoandika, ni Mwenyezi Mungu aliyeumba katika akili yake utashi wa kuandika. Wakati huo huo Mwenyezi Mungu hutoa uwezo wa kuandika, kisha huleta mwendo wa mkono na kalamu na mwonekano kwenye karatasi. Mambo mengine yote hayana hisia, ni Mwenyezi Mungu pekee anayetenda."

Je, huu ni kweli?

Kwa Kiarabu neno "qadar" (au "taqdir" kwa lugha ya kitheolojia) ni "kupanga tangu awali"; (linganisha pia na "kismet") limeonyeshwa katika Sura 9:51:

"Halitatusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu."



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 2 30-10-2021 20:52:02

Kwenye mabishano kati ya Adamu na Musa, yaliyotolewa kwenye Hadith ("Sahih Muslim", uk. 1396-1398), Musa anahojiana na Adamu kama ifuatavyo:

> "'Wewe ni baba yetu, ulituumiza na kusababisha tuondoke kwenye Paradiso.' Adamu alimwambia ... 'Unanilaumu kwa tendo alilonipangia Mwenyezi Mungu miaka 40 kabla ya kuniumba.' Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema (au akaongeza): 'Hivi ndivyo Adamu alivyokuja kuwa mbora wa Musa.'"

Abu Huraira alisimulia kuwa Mtume wa Mungu alisema hivi:

> "Mwenyezi Mungu amepanga uzinzi wenye kila mwanadamu atajihusisha nao, na ambao lazima ataufanya (au "hakuna kuukwepa")."
>
> (Taz. pia Mishkat, Juzuu ya 3, Sura ya 32:6)

Kulingana na Wasunni, Mwenyezi Mungu ameonyesha utashi Wake kwenye mbao zilizohifadhiwa mbinguni. Kurani pamoja na Hadithi, inasema wazi, kuwa mwanadamu lazima afanye kama alivyoamuru Mungu. Mungu ana hiari ya kuruhusu au kutoruhusu mtu kuingia peponi au kutupwa motoni:

> "Mwenyezi Mungu angalitaka kwa yakini angalikufanyieni kundi moja (Ummah). Lakini Anamuachia kupotea Anayemtaka. Na Anamwongoa Anayemtaka. Na hakika mtaulizwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya."
>
> (Sura 16:93)

Andiko hili lilizusha mabishano makali kati ya wale wanaoamini kuwa kila kitu kimeandikwa na Allah (Waasharia) na wale wanaoamini utashi huru wa mwanadamu (Waquadriya, baadaye Wamutazili). Baadaye Watazalite wakachukiwa kuwa si Waislamu kamili.

Mtume wa Allah alisema:

> "Kuna vikundi viwili vidogo kwenye kundi la wafuasi wangu visivyo na sehemu kwenye Uislamu - Wamurjiya na Waqadriya.



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 3 30-10-2021 20:52:02

Siku moja ardhi itadidimia na kutakuwa mabadiliko ndani ya wafuasi wangu, na hilo litakuwa kwa wale wasioamini kuamriwa tangu asili.

Msiwazoee Waqadriya na msiwatendee haki."

(Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:22-25)

Wanatheolojia wa Kimutazili walihoji kuwa kama kuna kuamuria tangu asili: "Kuna maana gani ya kuwapo amri, na makatazo, thawabu, na adhabu, vitisho na ahadi, manabii na vitabu?"

Kwa upande mwingine, Waasharia walidai kuwa mwanadamu amelazimishwa na nguvu ya amri ya Mungu ya milele na isiyobadilika afanye anayoyafanya. Mungu akitaka anaweza kuruhusu wanadamu wote waingie Peponi, au watupwe motoni. Wao hurejea kwenye ushuhuda wa Kurani:

"Sisi tumekiumba kila kitu kwa kiasi." (Sura 54:49)

"... Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuumbeni nyinyi na mnavyovifanya." (Sura 37:96)

"Amtakaye Mwenyezi Mungu humwacha kupotea; na Amtakaye humweka katika njia iliyonyoka."

(Sura 6:36 (38))

"Mwenyezi Mungu hufuta Ayatakayo na huthubutisha ayatakayo." (Sura 13:39)

## JE MUNGU ANAJALI?

Matokeo ya fundisho hili yameibua ile "sheria ya chanzo na matokeo", kuwekwa kando kuhusu suala la uadilifu. Ni Mungu peke yake anayesababisha mambo kuwa au kufanyika. Hivyo kimantiki mwanadamu hawezi kufanya mwenyewe jambo jema au baya. Hadithi moja inaeleza hivi:

"Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema - Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu aliukamata umma mmoja kwa



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 4 30-10-2021 20:52:02

mkono Wake wa kuume na umma mwingine kwa mkono wake mwingine, akasema: 'Huu ni kwa ajili ya hili, na huu ni kwa ajili ya hili, na sijali.' 'Sijui niko upande upi kati ya hizo mbili." (Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:32 (455w))

Bila shaka andiko hili linazungumzia Paradiso na Jahanamu.

Hadithi nyingine inaweza kuleta mshituko mkubwa hata zaidi:

"Mwenyezi Mungu alimwumba Adamu. Kisha alisugua bega lake la kulia na kutoa jamii nyeupe kama vile walikuwa mbegu, na akasugua bega lake la kushoto na kutoa jamii nyeusi kama vile yalikuwa makaa ya mawe. Kisha aliwaambia waliokuwa upande wake wa kulia: 'Nendeni Peponi na sijali.' Aliwaambia wale waliokuwa kwenye bega lake la kushoto: Nendeni motoni na sijali.'"

(Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:32 (454w))

Fundisho hili lilikujaje? Hadithi nyingine kutoka kwa Al-Bukhari inasema hivi:

"Mwenyezi Mungu alimwumba Adamu ... kutoka kwake akatoa jamii na kusema, 'Nimeiumba jamii hii ... iende motoni, na matendo yao yatakuwa kama yale ya watu wa motoni!' Kisha mtu mmoja akamwambia Nabii, 'Matendo ya namna yo yote yatakuwa na maana gani?' Akasema, 'Mwenyezi Mungu alipomwumba mtumishi wake kwa kwenda Peponi, matendo yake yatamstahilisha pepo hadi atakapokufa - na Mwenyezi Mungu alipomwumba mtu ili aende motoni, matendo yake yatakuwa kama ya watu wa motoni hadi atakapokufa na kuingia humo.'" (Al-Bukhari 87:6511, Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:4 na 14)

Hili linathibitishwa na Kurani:

"Tungalitaka Tungempa kila mtu uwongofu wake, lakini imehakikika kauli iliyotoka Kwangu: 'Kwa yakini Nitaijaza Jahanamu kwa wote hawa; majini na watu.'"

(Sura 32:13)



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 5 30-10-2021 20:52:02

Kuhusu wasioamini, tunasoma katika Sura 2:6, 7:

"Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye hawataamini. Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao."

Ikizungumzia wanadamu wote, inasema katika Sura 7:178, 179:

"Atakaowaongoza Mwenyezi Mungu ndio watakaoongoka; na Atakaowaachia kupotea ndio watakaopata khasara. Tumewaumbia moto wa Jahanamu wengi katika majini na wanadamu ..."

"Je! Mnataka kumwona mwongofu ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kuwa kapotea? Na aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwisha potea hutampatia njia." (Sura 4:88)

"Kama Mola wako angalipenda, Angaliwafanya watu wote kuwa umma mmoja. Kwa hiyo wataendelea tu kuhitilafiana. Kwa hiyo Mungu amewaumba. Na litatimia neno la Mola wako: 'Kweli kweli Nitaijaza Jahanamu kwa majini na binaadamu.'" (Sura 11:118, 119)

"Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea Amtakaye, na humuongoza Amtakaye." (Sura 14:4)

Kulingana na Sura 91:7, 8: "Mwenyezi Mungu aliitengeneza nafsi (roho), kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake."

"Basi Mwenyezi Mungu ndiye mwenye hoja ya kweli; na kama Angalipenda Angalikuongozeni nyinyi nyote." (Sura 6:149)



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 6 30-10-2021 20:52:02

## LIMEAMURIWA NA KUAMULIWA

Hadith ("Sahih Muslim", uk. 1395) inathibitisha maana ya aya hii:

> "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, una maoni gani kuwa wanayofanya watu duniani, na kuyatafuta, ni jambo lililoamuliwa kwa ajili yao, na hatima yao ya baadaye itaamuliwa na ukweli kuwa manabii wao waliwaletea mafundisho ambayo hawakuyatii, na hivyo WAKASTAHILI adhabu?" Juu ya hilo alisema: "Bila shaka linatokea kama lilivyoamuriwa na hatima na kuamuliwa kwa ajili yao, mtazamo huu unathibitishwa na aya hii ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Mkuu na Mwenye utukufu: 'Iangalie nafsi na Yeye aliyeithibitisha, kisha akapulizia ndani yake uovu wake na wema wake.'" (Mkazo wa Mwandishi)

Na katika Sura 5:20 tunasoma:

> "Mungu humsamehe Anayemtaka na humwadhibu Anayemtaka."

Hadithi inasimulia:

> " Nabii alisema: Ukisikia mlima kuwa umejihamisha kutoka mahali pake, amini, lakini ukisikia kuwa mtu amebadilisha asili yake, usiamini maana hilo litarudia mahali lilipoumbiwa."
>
> (Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:32 (458w)

> "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ninakuamini na ninaamini ulicholeta. Bado una hofu kwa ajili yetu? Alijibu, 'Ndiyo, mioyo iko kati ya vidole viwili vya Mwenyezi Mungu. Yeye hubadilisha anavyotaka.'"
>
> (Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:20)

> "Mwenyezi Mungu aliumba viumbe vyake gizani, kisha akaleta nuru yake juu yao, hivyo aliyepata cho chote kutoka kwenye nuru ile alipata mwongozo, na aliyekosa alipotoshwa." (Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:19)

“Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Toa taarifa kuhusu yale wanayofanya wanadamu na kuhangaika ndani hayo. Ni jambo lililoamuliwa juu yao na walilokuwa nalo kutokana na vipimo vilivyoamuliwa tangu asili, au kuhusu yatakayotokea baadaye kutokana na waliyowapa Manabii wao na hivyo uthibitisho umeonekana kwao? Alisema, ‘Hapana, bali ni jambo lililoamuliwa kwa ajili yao tangu asili na lililopita kwao; na uthibitisho wa hilo umo kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Mtukufu na Mweza wa yote: Na kwa roho na kwa yeye aliyeifanya kuwa kamilifu. Kisha kwa uvuvio aliionyesha wazi ilivyoikiuka kweli, kadhalika na ilivyotenda wema.”

(Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32: 7)

“Hakika yake Mwenyezi Mungu mweza yote na aliye Mtukufu alikamilisha mambo matano kwa kila kiumbe Wake mwanadamu: muda wake ulioamuliwa, UTENDAJI wake, mahali pake pa kupumzikia, mwenendo wake na mahitaji yake.” (Mishkat Juzuu ya 3, Sura ya 32:32)

## UKIUKAJI WA HAKI?

Tunaamua hili kuwa ni kusudi. Mwanadamu huhukumiwa kwa kile anacholazimika kukifanya. Kwa kweli huu ni ukiukaji kamili wa haki. Tusipuuze kauli zote hizi.

Kuwa Mwislamu huashiria kukubaliana na kuchaguliwa tangu asili. Mwislamu wa kweli anapaswa kuwa tayari kustahimili hukumu, na Mwenyezi Mungu akipenda kumhukumu tena kwa sababu ambazo hazikubainishwa, anapaswa kuwa tayari kuipokea hukumu hiyo. Huenda tunapaswa kukumbuka kuwa neno lililotumiwa kwa maana ya kuchaguliwa au kuamuliwa tangu asili, kwenye Uislamu haliashirii kujulikana tangu asili, bali tu kuamuriwa na kuamuliwa tangu asili!

Mwanatheolojia maarufu wa Kiislamu, al-Ghazzali amesema hivi:



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 8 30-10-2021 20:52:03

*"Haki ya Mungu isilinganishwe na haki ya mwanadamu ... Hakuna cha kumlazimisha afanye, wala kudhaniwa kuwa amekiuka haki, wala hawezi kuwajibishwa na mtu ye yote."*

Ibn-Hazm pia alikuwa na maoni kama hayo:

*"Ingawa Kurani hutumia jina la Allah linalomaanisha 'mwenye rehema kuliko wote wanaoonyesha rehema', neno hilihalimaanishi kuwa ni mwenye rehema jinsi tunavyolielewa neno hili, maana ni dhahiri kuwa Mwenyezi Mungu si mwenye rehema. Yeye huwatesa watu wake na kila aina ya magonjwa, vita na huzuni. Hivyo basi Kurani ina maana gani? Maana ya "mwingi wa rehema" ni moja tu , ya majina ya Mungu. Jina hili halikusudiwi kuionyesha asili yake. Lazima tulitumie kwa sababu Kurani hulitumia, lakini tusijifanye kuwa tunaielewa maana yake."*

Neno hili lililotumiwa kwenye kurani huenda lilikuwa na maana tofauti wakati ule, ambayo kwa kweli siku hizi hatuwezi kulielewa.

Hata hivyo lazima tulitumie neno hili, kwa sababu hatuwezi kuyabadilisha maneno ya Kurani."

Tatizo linalojitokeza ni jepesi na la wazi. Ikiwa katika Kurani Allah anajidhihirisha kama Mungu wa kiholela anayefanya anavyopenda, bila ya mishikamano yo yote hata kwenye misemo yake mwenyewe, anaongeza wazo geni kabisa kwenye mafunuo ya awali, ambayo Muhammad alidai kuyathibitisha, na ambamo tunahimizwa kumchukulia Mungu kwa kulikubali Neno Lake.

Lazima tutambue kuwa Mungu ni mwenye msimamo, ni wa haki na ni mtakatifu. Ukiwa na dosari yoyote au kupingana katika maandiko yanayodai yametoka kwa Mungu, mwanadamu ndiye wa kulaumiwa, si Mungu. Haikubaliki kuficha haya ili kulinda kitabu au nabii, au dini na viongozi wake.



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 9 30-10-2021 20:52:03

## JE, HAKUNA NJIA YA KUMFIKIA MUNGU?

Mpendwa msomaji, kama yaliyonukuliwa hapa ni mapya kwako, basi huenda huna ufahamu wa Kurani (na umeyakabidhi maisha yako ya milele kwa watu wengine wasio na ufahamu); au umo mikononi mwa viongozi wanaojua ukweli huu lakini wameuficha usiupate.

Ninafikiri sote tunakubaliana kuwa mwanadamu ana uhuru wa kuchagua. Ingawa huenda tusipende wazo la kuchagua, inaonekana kuwa na chaguo tu la kushuka chini . Wote tunatambua kwa uchungu kuwa maazimio ya Mwaka Mpya, au hasa maazimio yote, hayatimizwi. Tuwe wa kweli. Tunatamani kuwa safi - lakini hatuko vile. Tunajitahidi kutenda kwa usahihi - lakini daima tunafanya makosa. Tunaweza kuwa wazuri, tukatekeleza wajibu wetu wa kidini "tukawa wazuri". Mungu anatuangalia kwa njia tofauti. Kwa kweli hatuwezi kumfikia Mungu, isipokuwa yeye atuvute. Hatuwezi kutenda mema, isipokuwa Yeye atende ndani yetu. Hiyo ni sehemu ya neema ya Mungu. Hata hivyo lazima ijulikane kuwa tukitumia maneno 'safi' na 'sahihi', hatupaswi kutumia viwango vya wanadamu, bali vya Mungu.

Tukikubali kuwa kila siku tumevunja sheria, maagizo na matarajio ya Mungu, itabidi tukabiliane na wajibu wetu na matokeo yake. Asili yetu iliyo dhaifu hufanya isiwezekane sisi kuwa na haki mbele za Mungu. Je,hakuna jibu , hakuna ukombozi?

## TUNAWEZAJE KUKUTANA NA MUNGU ALIYE MTAKATIFU?

Hii inategemea jinsi 'tunavyomwona' Mungu. Yeye ni mwenye haki na ni Mtakatifu - au ni mwenye rehema, msamaha na fadhili? Kwa kuangalia mara moja, tutasema kuwa yeye ana yote hayo. Na hilo ni kweli! Lakini haki na utakatifu haviwezi kupatana na dhambi. Hatuwezi kuingia kwenye uwepo wa Mungu ulio mtakatifu kama tulivyo! Kama moto usivyoweza



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 10 30-10-2021 20:52:03

kupatana na maji, utakatifu wa Mungu hauwezi kupatana na upotovu wetu. Tusijipumbaze kwenye jambo hili!

Msamaha haufanyi kazi kiuchawi. Siyo kwamba Mungu husahau tu kuhusu hayo. Dhambi ni chukizo kwa Mungu kiasi kwamba inabidi aishughulikie kwa hukumu ya haki! Lakini haki ya Mungu na upendo wake kwetu vinawezaje kukutana? Tukio kutoka kwenye historia linaweza kulifafanua jambo hili:

Shamueli alikuwa Mfalme wa Caucasia aliyeishi mamia kadhaa ya miaka ya nyuma. Watu wake walikuwa katika vita vya kudumu na Waturuki. Aliwahi kuuzingira mji mmoja wa Waturuki akiwa na jeshi lake. Kama kawaida mama yake alikuwa naye katika kambini. Usiku mmoja alipanga shambulio la kushitukiza, lakini adui alikuwa macho akimsubiri. Mipango yake ya siri ilikuwa imesalitiwa. Kwenye vita hivyo walishindwa. Kwa hasira Shamueli alitangaza kuwa msaliti aadhibiwe, kwa kuchapwa viboko mia akigunduliwa. Tena kwa siri kubwa shambulio lingine lilipangwa. Matokeo yalikuwa yale yale. Lakini msaliti aligunduliwa. Alikuwa mama wa Shamueli.

Kwa siku tatu mchana na usiku alijitenga akawa hemani kwake. Afanye nini? Akimwacha huru mama yake, wote watakuwa na haki ya kusema kuwa hatendi haki. Hata hivyo akimwadhibu wote watasema: ‘Mwone Shamueli! Hana huruma hata kwa mama yake!’ Mwishowe alijitokeza. Jeshi lake lilikusanyika likitarajia hukumu itolewe bila kujua itakuwaje. Kwa taadhima aliwahutubia watu wake: ‘Mara mbili tumeshindwa kwenye vita kwa sababu ya usaliti. Watu wetu wameuawa. Kosa lilitendeka, hivyo lazima adhabu itekelezwe kulingana na sheria yangu - kwa viboko 100! Haki na hukumu lazima vidumishwe.’

Mama yake alileltwa. Alionekana mdhaifu huku akitetemeka kwa hofu. Mtekelezaji wa adhabu aliinua mjeledi wake - lakini kabla ya kiboko cha kwanza, Shamueli alipiga kelele: ‘Subiri - Huyu ni mama yangu. Mimi ni sehemu ya mwili na damu yake. Nitaichukua adhabu kwa ajili yake!’ Aliingia kwenye mzunguko, akavua vazi lake na kuagiza: ‘Chakari, chapa ukitimiza wajibu wako kama ilivyo kwa wengine bila ya huruma.’ Viboko vyote



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 11 30-10-2021 20:52:03

alivipata, moja baada ya kingine hadi akazimia, kwa bahati nzuri alinusurika kwenye matarajio mabaya yaliyokuwako.

Tukio lile ambalo huenda linazidi lingine lo lote katika historia, linafaa kwenye mfano wa Yesu. Yeye alikuwa Mungu katika namna ya mwanadamu. Ilibidi na inabidi atekeleze hukumu ya haki. Lakini katika upendo wake wa kweli, Alijitwika dhambi zetu - zangu na zako, akapata mateso makali msalabani badala yetu.

Hata hivyo tunatambua kuwa ukatili haukuwa tu ule wa mwilini, bali kwamba Mungu aliye mtakatifu alijitwika mwenyewe adhabu ya dhambi zetu.

Haki na upendo vilikutana kwenye msalaba wa Yesu.

"Kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao".(*2* Wakorintho 5:19)

Tukio hili lilitokea mara moja tu. Sadaka hii kwa ajili ya dhambi inatosha watu wote, wakati wote. Ni neema ya Mungu, karama ya Mungu kwetu ambayo hatukuistahili. Hata hivyo karama hiyo ni yetu tu tukiipokea na kuitunza!

Nikimletea dhambi zangu zote kwa uaminifu katika maombi ya toba, nitasafishwa:

> *... nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena.* (Yeremia 31:34)
>
> *... [utayatupa) maovu yetu yote katika vilindi vya bahari.* (Mika 7:19)
>
> *Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, ndivyo Mungu alivyoziweka dhambi zetu mbali nasi.* (Zaburi 103:12)
>
> *Kama tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha kutoka kwenye udhalimu wote.* (1 Yohana 1:9)

Ninaamini kabisa kwamba hakuna mtu, baada ya kutambua hasa Yesu ni nani na amefanya nini, anayeweza kumwomba Mungu msamaha kwa juu juu tu bila ya majuto halisi kwa



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 12 30-10-2021 20:52:03

athari tuliyoileta kutokana na utashi wetu binafsi; kumtesa Yesu msalabani. Hata hivyo baada ya kulitambua hili mtu ANAWEZAJE tena kufikiria dhambi moyoni mwake? Ndiyo, Tunaweza kubabaishwa. Tunaweza kuanguka. Lakini hatutaki kutafakari na kupanga matendo yatakayomwumiza Mungu.

## MIKONO YA MUNGU IKO WAZI KABISA

Huu ndio msimamo tunaoweza kuweka tunapoomba msamaha. Kwenye mfano wa 'Mwana Mpotevu' (Luka 15:11-32), Yesu anazungumzia mtu aliye na wana wawili. Mmoja alichukua sehemu ya urithi wake akaenda mbali na kuutapanya huko, hadi akautumia wote. Akiwa kazini kwenye shamba la nguruwe, ndipo *alipozingatia moyoni mwake*. Aliikadiria hali yake kwa uzito na uaminifu. Ilibidi atafakari baada ya maisha kuwa magumu. Biblia ina neno hili lililotafsiriwa kuwa ni 'toba'.

Lilikuwa hivi: Yule kijana aliazimia.

*a. Nitaondoka*

*b. Na Kurudi kwa baba yangu*

*c. Na kumwambia, 'Baba, nimetenda dhambi mbele za Mungu na mbele yako. Sistahili tena kuitwa mwanao.'*

Alichotaka ni kuwa tu mtumishi kwa Baba yake, badala ya kutumikia mgeni kwenye shamba la nguruwe, kwa sababu alikaribia kufa kwa njaa. Azimio hili lilikuwa zuri sana. (Huenda tumewahi kufanya azimio kama hilo hapo nyuma.) Lakini hilo halikutosha. Kijana kwenye mfano wetu hakukomea hapo bila ya kulitimiza azimio lake:

*d. Akaondoka akaenda*

*e. Kwa Baba yake*

Alishangaa kuona kuwa kumbe Baba yake alikuwa akimtafuta. Cha kushangaza zaidi, Baba yake alikuwa bado akimtambua. Mwanzoni kijana aliondoka akiwa na tumaini, lakini matarajio yake ya maisha ya furaha ya kweli yenye mafanikio hayakupatikana. Alirudi akiwa kama ombaomba mchafu anayenuka. Lakini cha kushangaza hata zaidi, Baba yake



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 13 30-10-2021 20:52:03

alimkimbiliiia akakutana naye, akamkumbatia na kumbusu! Hata kabla ya huyo mwana kukiri kikamilifu makosa yake, Baba yake,

1. alimvika (alifunika uchafu wake. Kwa Kiebrania neno lile linatokana na msingi ule ule kama 'upatanisho' = kupatanisha kwa njia ya sadaka) *joho lililo bora sana*,
2. kisha akaamuru *tieni pete kidoleni mwake* (yaani muhuri unaoashiria kukubaliwa kwake tena kama mwana),
3. *na viatu miguuni mwake* (walioruhusiwa kuvaa viatu ni wale tu walio huru).
4. Kisha aliagiza iandaliwe sherehe, *'Kwa maana huyu mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai; alikuwa amepotea naye amepatikana!'*

Bila shaka kurudi nyumbani lilikuwa jambo gumu sana. Hata hivyo ukiisha kuifanya toba kuna furaha ya ajabu kabisa. Baba yetu hatazikumbuka dhambi zetu tena! Hakutakuwa na maswali ya kuaibisha Siku ya Hukumu. Imepitishwa na kuisha.

Lakini kumbuka kuwa Baba alikuwa na wana wawili. Yule mwingine aliporudi nyumbani kutoka shambani na kusikia kelele za sherehe na kuambiwa kuwa ilikuwa kwa ajili ya ndugu yake, alikasirika. Hakutaka kujiunga kwenye sherehe pamoja na *'huyu mwanao'*. Wakati wote huyo mwana mkubwa alikuwa nyumbani akimtumikia Baba yake na haikuwako sherehe yo yote kwa ajili yake! Hakusherehekea kamwe lakini angeweza kusherehekea! Aliona kuwa sifa yake ya kuwa mwana ilikuwa mzigo. Huyo anamwakilisha mtendaji wa kidini anayefanya wajibu wake, lakini moyoni mwake hajaridhika.

**Kwa uaminifu kabisa, ni yupi kati ya hao wawili huwakilisha hali yako wewe binafsi?**

Inahitaji aina mpya ya maisha ili uweze kutembea na Mungu. Mungu analijua hili na hulikimu pia. Yesu alisema:

"Amin, amin, nakuambia hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa mara ya pili." (Yohana 3:3)



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 14 30-10-2021 20:52:03

Kuzaliwa Upya ndio mwanzo wa hayo Maisha Mapya, na hufuatiwa na mchakato wa ukuaji. Toba, Kuzaliwa Upya na kuokoka vinaweza kutokea ndani ya saa moja. Maisha ya Kikristo yanapaswa kukua hadi atakapoiacha dunia hii.

Badiliko hili ndani ya mtu ndiko hasa ‘kuokoka’ (kuokoka = kubadilika). Huanza tunapouona upumbavu wa maisha yetu yenye ubinafsi tukatamani kuishi kwa namna inayompendeza Mungu. Ikiondoka chembe ya dhambi iliyotutenganisha na Mungu, Yeye huanza kuwasiliana na mwanadamu, aliyekuwa amekufa na yuko hai tena.

*... mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu.*

(Waefeso 2:1)

Mchakato wa ‘kuhuisha tena’ huitwa ‘Kuzaliwa Upya.’ (Yohana 3:3-5). Bila shaka huu hauwezi kuletwa na mwanadamu. Ni uingilianaji wa kimungu.

Dini inaweza kuzaa aina zote za namna za kimaadili na kidesturi zinazoweza kutiishwa na hofu ya adhabu au shinikizo la kijamii. Lakini kwa kuzingatia sheria hizi, hata zikiwa nzuri kwa kuushinda uovu, huleta utumwa na kuvunja moyo upendo. Ubora wa maadili hauji kwa kushinda tendo la uovu, bali hupatikana kwa kuuchukia uovu kwa vile ulivyo.

Kwa nje jamii Iliyo chini ya sheria za kidini huonekana kuwa safi zaidi kimaadili, lakini asili ya moyo wa mwanadamu hubaki bila mabadiliko, na moyo safi ndio anaotafuta Mungu.

Mungu anataka abadilishe, dhamira na azma (yaani ‘moyo’) wa mwanadamu. Mungu anatafuta ndani yetu moyo ulio safi - kwa sababu anataka aishi ndani yetu!

Wale wanaoitikia upendo wa Yesu ndio wanaolijenga kanisa la kweli. Halijaimarishwa ipasavyo, lakini lipo duniani kote ingawa ni kwa walio wachache. Ndani yake na kutoka humo sharti tuione kanuni hii ya upendo ikielekezwa kwenye uwiano wa mtu kwa mtu. Mchakato huo hautakamilika, kwa sababu ya bidii ya mtu, au kwa hofu ya kupoteza kitu wanachoweza kupata au kufurahia, kila mara watakuwa wakijiondoa kwenye Ufalme wa Mungu. Huu ndio upande wa kuhuzunisha wa



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 15 30-10-2021 20:52:03

uhuru ambao Mungu amempa mwanadamu. Hata hivyo bila uhuru huu, mwanadamu atakuwa kama roboti lililopangiliwa.

Huenda ungependa kuuliza kwa nini kuna walevi wengi sana kati ya Wakristo; kwa nini kuna upotovu na kukosa maadili na unyonyaji mwingi. Jibu liko wazi sana.

> *"Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni."* (Mathayo 7:21)
>
> Haya ni maneno ya Yesu.

## MTU ALIYEPOKEA MSAMAHA

Si kila chupa yenye nembo ya 'Coca Cola' huna na kinywaji hicho. Kuna chupa zilizo tupu, zingine hazitumiki, zinaweza kujazwa hata pombe kali na mafuta ya taa. Kibiblia, Mkristo, ni mtu aliyepokea, kwa moyo uliovunjika na wenye shukrani, karama ya msamaha kama ilivyoelezewa hapo juu, na ambaye basi anaishi katika ushirika hai na Bwana wake katika kujisalimisha kwake kikamilifu.

Yote haya huenda yakawa mageni kwako, kama wewe ni Mwislamu. Lakini lazima tuwe wazi kabisa juu ya hili: **bila ya sadaka haiwezekani kuwako njia ya kupatanisha haki na rehema.** Na Uislammu hukanusha uwezekano wo wote wa msamaha wa dhambi zetu kwa njia ya sadaka.

Kinyume na "vitabu vilivyofunuliwa mwanzoni" 'moyo' wa Mwenyezi Mungu hauhusiki katika theolojia ya Kiislamu, kama Al-Barkhavi anavyosema:

> "Kama makafiri wote wangekuwa waumini, Mwenyezi Mungu hangepata faida yo yote. Kama waumini wote wangekuwa makafiri, hangepata hasara."
>
> Al-Ghazzali analithibitisha hili:
>
> "Upendo ni kuhisi hitaji la kupendwa na kwa kuwa haisemekani kuwa Mwenyezi Mungu analo hitaji wala uzoefu wa hitaji, kwa hiyo haiwezekani Mwenyezi Mungu kupenda."



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 16 30-10-2021 20:52:03

Linganisha hili na ujumbe wa Yesu aliyesema kuhusu yeye mwenyewe:

> *“Mimi ndimi mchungaji mwema. Ninawajua kondoo wangu nao kondoo wangu wananijua. Kama vile Baba anavyonijua mimi, nami ninavyomjua Baba, nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo. Ninao kondoo wengine ambao si wa zizi hili, inanipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti yangu, hivyo patakuwa na kundi moja na mchungaji mmoja.*
>
> *Baba yangu ananipenda kwa kuwa ninautoa uhai wangu ili niupate tena. Hakuna mtu aniondoleaye uhai wangu, bali ninautoa kwa hiari yangu mwenyewe. Ninao uwezo wa kuutoa uhai wangu na pia ninao uwezo wa kuutwaa tena. Amri hii nimepewa na Baba yangu.”*
>
> (Yohana 10:14-18)

## NI JUU YAKO KUFANYA UAMUZI HUO

Kwenye Biblia tumeagizwa kuchagua tutakayemtumikia (Yoshua 24:15). Hili linataka uamuzi baada ya kutafakari kwa busara na kikamilifu. Kumchagua Mungu ni kuchagua njia yake na Neno lake kama msingi wa ufahamu na kuamini. Kuamini Neno la Mungu ni kuamini ahadi zake na kufanya mapenzi Yake. Kuamini huku pamoja na matokeo yake ya vitendo huitwa imani.

Biblia inatufundisha wazi kuwa ni imani ya Abrahamu, Musa na wengine wote wenye sifa, iliyowafanya wakubaliwe na Mungu. Na ilikuwa, na hata leo, ndiyo imani hii peke yake iliyohesabiwa na inayohesabiwa kwao na kwetu kuwa ni haki. (Waebrania 11, Warumi 4: 18-25, Mwanzo 15:6).

Hivyo haki inayohitajika ili tuingie kwenye uwepo wa Mungu si matokeo ya juhudi zetu ya kujaribu kurekebisha dosari kwa kumfanyia Mungu matendo mema kama malipo.

Hakuna ustahili katika kutimiza wajibu wetu! Haki ni yetu tu Mungu anapotutangaza kuwa ni wenye haki.



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 17 30-10-2021 20:52:03

Imani huikubali njia pekee ya Mungu ya upatanisho. Ametamka kuwa hakuna mtu anayeweza kuokolewa kutoka kwenye hukumu ijayo isipokuwa kwa kuikubali karama yake: Msamaha kwa njia ya Yesu. Yesu alisema kuhusu yeye mwenyewe:

*"Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu* [kujua maana soma Danieli 7:13] *hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia* [= malipo ya kumweka huru mtumwa] *kwa ajili ya wengi."* (Marko 10:45)

Yesu alisema pia:

*"... Hii ndiyo damu yangu ya agano,* [nayolithibitisha agano kati ya Mungu na watu wake] *imwagikayo kwa ajili ya wengi."* (Marko 14:24)

Baadaye kidogo Mtume Petro alisema hivi kuhusu Yesu:

*"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna jina jingine* [Mungu hakutoa jina jingine] *chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."* (Matendo 4:12)

Haya yanaelezea Jina la Yesu (Kiebrania - Yeshuah = wokovu).

Alikuwa akilithibitisha tena alilowahakikishia Yesu wanafunzi wake, maana Yesu alisema:

*"Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu."* (Yohana 14:6)

Bila shaka tutataka kuhoji: "Kwa nini Mungu alilifanya kwa njia hii na si nyingine?" au "Itakuwaje Mungu kufa kwa ajili ya wenye dhambi wasiostahili?" Lakini sisi ni nani hata tumhoji Muumba wetu? Mungu amesema! Na kwa hiyo alilosema linasimama. Na Neno lake linaungwa mkono na ushahidi wa kutosha na wa kuthibitishwa kuwa unatoka kwa Mungu. (**Tafadhali andika uagize kijitabu chetu JITAHIDI KULINGANISHA ili upate zaidi kuhusu somo hili**).

Mpendwa msomaji, hili linakuacha ukiwa na uamuzi ambao hakuna atakayekufanyia na ambao huwezi kuuepuka:

Kama utachunguza kwa dhati na uwazi, au la, kauli zilizomo kwenye kitabu hiki.  Bila shaka unapaswa kuiangalia mitazamo ya pande zote. Yaangalie mambo yote pamoja na ushahidi unaounga mkono, unaotumia maandishi yenye maarifa zaidi, tunayoyatoa kwa furaha bila malipo kwa ye yote anayeyatafuta kwa dhati. Tunakuhimiza pia ulisome Agano Jipya ukiwa na ari ya kumwomba Mungu akufunulie hiyo kweli ya Mungu.

Huu ni wajibu wako mtakatifu mbele za Mungu, ... *anayetaka watu wote waokolewe na wafikie kuijua kweli.* (1 Timotheo 2:4, 2 Petro 3:9).

Ni upumbavu hasa kutoa hoja kuwa anavyofikiri na kuamini mtu ni sahihi, bila ya kuwa umejaribu na kupima kwenye uhalisi na ukweli. Ni karibu na wazimu kutegemea mambo ya kusikia linapokuja suala la ni kweli au si kweli kuwa tutaishi milele kwenye uwepo wa Mungu Mweza wa yote, au tutaishi motoni.

Usibahatishe huu, “Huenda” ukawa uamuzi wako wa mwisho!



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd   19    30-10-2021   20:52:03

**Mpendwa Msomaji,**

Wote tunajua inavyoshawishi kuyasukuma mambo hadi wakati ulio bora. Tunasema, "labda kesho", lakini kesho huenda isije kamwe. Tunakuhimiza moyo uchukue muda SASA kujibu maswali haya:

1. Kwa nini ni muhimu kabisa kuwa na "mtazamo ulio wazi" kwenye suala la majaliwa ya mwanadamu?
2. Kwa nini suala la "Utashi Huru" ni muhimu sana kwetu?
3. Unakubaliana na hitimisho la mwandishi kuwa Kurani hushikilia fundisho la "ushupavu kamili"? Au unaweza kupendekeza maelezo mengine?
4. Unachukua msimamo gani kwenye Hadithi na nukuu zilizotolewa kwenye sehemu ya mwanzo ya kijitabu hiki?
5. Elezea kauli ya ukurasa wa 7: "Kwa kweli, hatuna njia ya kumfikia Mungu, isipokuwa yeye hutuvuta sisi."
6. Kwa nini msamaha hauwezi kufanya kazi kimaajabu?
7. Na kwa nini kutambua kwetu kuhusu Yesu ni nani na amefanya nini kuna athari kwenye msimamo wetu juu ya dhambi?
8. Yule kijana kwenye mfano wa 'Mwana Mpotevu' alichukua hatua zipi ili kurudisha uhusiano na baba yake?
9. Tunajifunza nini kutoka kwenye mfano huu?
10. Kwa nini dini kama ilivyo haitoshi kumrudisha mwanadamu kwenye ushirika na Mungu?
11. Mwandishi anauelezeaje ukweli kuwa kuna ulevi, ukosevu wa maadili na uovu mwingine kwa wengi wanaojiita Wakristo?
12. Uamuzi wetu utawaliwe na nini kuhusu nani tutamtumikia kwa maisha yetu?

Tuma majibu yako na maoni yo yote kwetu.

Asante.

Kumbuka ofa yetu: Bado tuna zaidi kwa ajili yako ili usome!



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 20 30-10-2021 20:52:03

**Vijitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya wasomaji wetu:**

1. Umeumbwa kwa Kusudi
2. Jitahjadi Kulinganisha
3. Mwisho Usiojulikana
4. Mpendwa Abdallah
5. Mtu mwenye Ujumbe
6. Kwa nini Kuiamini Biblia
7. Kurani na Biblia
8. Fuata Moyo wako

Al-Kitab - *Kitabu cha Vitabu* (Kozi ya Biblia)

*Tafadhali nitumie* ....................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

Tuma barua yako kwa:

**Hamasa ya Milele**
S.L.P. 11795
Arusha, TANZANIA
hymilele@gmail.com

**Life Challenge**
S.L.P. Box 50770- 00200
Nairobi, KENYA
info@lifechallenge.de



03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 21 30-10-2021 20:52:03

03DestinationUnknown-Swahili -Edited by SB.indd 22 30-10-2021 20:52:03